

**MARCIDES**  
**MARCIDES & CO**  
**LAW OFFICE**

Nicosia, Desemba 14, 2015

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Cyprus

Mr. Nicos Anastasiades,

Makazi ya Rais, Nicosia

Mheshimiwa Rais,

**BARUA YA WAZI**

Nikiwa kama mshauri wa kisheria wa wamiliki wa BENKI ya FBME, Mabwana. Ayoub-Farid Michel Saab na Fadi Michel Saab, nina maelekezo ya kukuletea barua hii kama Mkuu wa nchi na kwa kutaja vifungu husika vya Katiba, ambayo hutoa mamlaka ya utendaji (Ibara ya 46 ya Katiba).

Inajulikana kwamba Benki Kuu ya Cyprus ("CBC") aliamua, katika nafasi yake kama Mamlaka ya Azimio, kwa maoni na kwa kulingana na tangazo lililotolewa na Idara ya Financial Crimes Enforcement Network ya Marekani ("FinCEN") Julai 2014 kuhusiana na BENKI YA FBME tawi la Cyprus ("Tawi"), kuliweka Tawi chini ya azimio kwa haraka ili kuziua shughuli zake, kwa kutoa amri 356/2014 ("Amri") kwa idhini ya Waziri ya Fedha.

Lengo kuu la Amri lilikuwa uuzaji wa shughuli za Tawi. Ingawa ilionekana tangia mwanzo kwa kuonywa kwamba hili haliwezi kutekelezeka, Benki Kuu iliendelea kulisitiza, kwa nafasi yake kama Mamlaka ya Azimio, kuendelea na utekelezaji wa Amri hiyo. Ingawa lengo la Amri lilikuwa kulinda maslahi ya wateja wa Tawi, ambao hawakuwa hatarini wakati huo, hata hivyo, imesababisha uharibifu mkubwa kwao.

Kabla ya kutolewa kwa amri na kufuatia utoaji wake, BENKI YA FBME na wamiliki wake walikuwa wakitoa maelezo muhimu mara kadhaa kwa Mamlaka ya Marekani pamoja na Benki Kuu, kupinga usahihi wa ripoti ya FinCEN kwa wakitumia ripoti iliyotayarishwa kwa niaba yake na makampuni yenye sifa ya kimataifa (Ernst & Young na KPMG ya Ujerumani).

Pia Benki ya FBME inauliza uhalali wa azma ya CBC kufanya uamuzi kwa misingi ya FinCEN wakati matokeo ya kesi katika Mahakama ya Marekani, ambapo amri ya mpito ya mahakama ilitolewa tarehe

27/08/2015, kuahirisha maamuzi ya FinCEN hadi hapo Mahakama itakapotoa uamuzi wake. Pamoja na hayo, CBC, ikiwa kama Mamlaka ya Azimio, haikuweza hata kidogo kubadilisha mwenedo wa matendo yake.

Kwa kuzingatia kwamba uamuzi wa FinCEN ulikuwa si sahihi kisheria, wamiliki wa FBME walijaribu mara kadhaa kufanya makubaliano na CBC kwa kuleta mapendekezo kwa CBC ili kukabiliana na hali hiyo, ambayo si tu iliathiri uaminifu kwa mfumo wa kibenki na uchumi wa Cyprus kwa ujumla, lakini pia uliathiri idadi kubwa ya wateja, waliopo kisiwani Cyprus. Kwa bahati mbaya, CBC, kama Mamlaka ya Azimio, si tu walikataa na kupuuza jaribio lolote la upatanishi, ambao ungeweza, kwa vyovyote vile, kupunguza kiasi cha madhara yaliyokwifanywa, lakini waliepusha njia yoyote ya mawasiliano, kwa kufanya ukandamizaji, usaliti, na wakati huo huo kutishia kuwawekea vikwazo vya kiutawala na kuwatoza faini na kuwafungulia kesi za jinai.

Kufuatia mwenendo huu wa CBC, kama Mamlaka ya Azimio, wamiliki wa BENKI ya FBME, ambao ni raia wa Lebanon, walifungua kesi ya usuluhishi dhidi ya Serikali ya Cyprus kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi mjini Paris (ICC Paris). Msingi wa shitaka hili ni Mkataba baina ya nchi mbili za Cyprus na Lebanon kuhusu ulinzi wa uwekezaji. Wadai hawa wawili ambao ni wamiliki wa BENKI ya FBME pamoja na mambo mengine, wanadai fidia dhidi ya Jamhuri ya Cyprus kwa madhara waliosababishiwa kutokana na vitendo vya CBC, kama Mamlaka ya Azimio.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali anawakilisha Jamhuri ya Cyprus katika usuluhishi huu. Pingamizi la Jamhuri ya Cyprus, kwamba Mahakama hii haina mamlaka ya kusikiliza shauri hili, lilitupiliwa mbali na kesi kuendelea hadi hukumu itakapofikiwa.

Mahakama hiyo ya Usuluhishi ya Kimataifa, imeiagiza Jamhuri ya Cyprus, kupitia Agizo No. 3 lililotolewa 13/05/2015 katika mwendelezo wa kesi hii:

*"... kujiepusha na kuchukua hatua yoyote itakaharibu biashara ya FBME Cyprus wakati tukisubiri kukamilika kwa usuluhishi huu, na kuamriwa kuwataarifu mwezi mmoja kabla Mahakama ya Usuluhishi, Wadai, Kiongozi wao Bw Mafuru na wengine wote wenye mamlaka wahusikao na shauri hili, na / au taasisi yoyote yenye mamlaka ..."*

Zaidi ya hayo, mahakama ya usuluhishi imeipa Jamhuri ya Cyprus Agizo jingine la tarehe 12/10/2015:

*"kuhakikisha kuwa hatua yoyote kuhusu FBME Cyprus inachukuliwa baada ya mdai kufanya tathmini ya kutosha ya umuhimu wake na uharaka katika utekelezaji kamili wa majukumu ya kimataifa ya mshitaki kulingana na mkataba wa Cyprus-Lebanon BIT. "*

Mheshimiwa Rais,

Pamoja na kuwepo kwa shitaka hilo na maagizo yake ya kiutaratibu, uamuzi wa zuiio la muda wa Mahakama ya Marekani na mambo mengine, CBC, kama Mamlaka ya Azimio, anasisitiza na inaendelea kuchukua hatua kiholela, kinyume cha sheria na kuwaumiza wamiliki wa BENKI ya FBME, wateja wa Tawi hilo, Jamhuri ya Cyprus na walipa kodi wake. Matokeo yake, Jamhuri ya Cyprus ndiyo itakayolipa madai yote yatakayotolewa na mahakama hiyo ya usuluhishi ambayo yanaweza kuwa makubwa na raia wake / walipa kodi wakielemea tena kwa mara nyingine.

Zaidi, utekelezaji wa uamuzi unaodaiwa na CBC, kufuta leseni ya Tawi kufanya kazi, itasababisha tukio lenye madhara yasiyoelezeka. Msugvano huu, yaani kushindwa kuuza kwa Tawi ambako sasa

Mamlaka ya Azimio inakiri yenyewe, ambayo kwa bahati ni CBC yenyewe. Matokeo yake, badala ya wale waliotoa amri kuwa majasiri kueleza kushindwa kwao na kubatilisha uamuzi huo, wanaendelea kuficha makosa yao kwa kusimamisha leseni ya Tawi, ambayo itapelekea matokeo mabaya sana kwa wote na hasa wateja wa Benki.

Mheshimiwa Rais,

Wewe ni Mkuu wa Nchi, Uliyepewa mamlaka na Katiba kuendesha nchi. Matatizo ya kesi hii hayakutokea CBC kwa nafasi yake bali yametokea CBC kwa nafasi yake kama Mamlaka ya Azimio, uwezo ambao hautokani na Katiba, bali kwa sheia Ndogo ya nchi, ambayo nayo imekuwa ikifanyiwa marekebisho mara kwa mara. Janga hili, ambalo lilianza kwa utoaji wa amri ya awali, ambayo hadi sasa inaendelea kufanya kazi, ilitolewa kwa idhini ya Waziri wa serikali. Amri kama hiyo isingeweza kutolewa bila ridhaa hii, ambayo iliwekwa kwa kutia saini chini ya maneno "nakubaliana".

Zaidi ya hayo, utetezi, ya Jamhuri ya Cyprus katika katika kesi hii ya usuluhishi haupo kwenye mamlaka ya CBC, bali kwenye mamlaka ya Jamhuri ya Cyprus, ambayo wewe ni mkuu wake. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni afisa wa kujitegemea wa Serikali, lakini anawajibika kwenye maelekezo ya Serikali ya Jamhuri ya Cyprus kuhusu ukweli na uhalali wa utetezi wowote atakaoutoa wakati akishughulikia kesi dhidi ya serikali.

Kwa yaliyojiri hapo juu, Tunakuomba kuitisha mkutano wa wadau wote wanaohusika (Waziri wa Fedha, Wajumbe wa Mamlaka ya Azimio na wamiliki wa BENKI ya FBME) chini ya urais wako ili kujadili uwezekano wa kutafuta ufumbuzi bora kwa ajili ya kulinda maslahi ya pande zote zinazohusika, ikiwa ni pamoja na Wateja wa Tawi, waliotajwa kulindwa na Azimio hili,

Wako Mtiifu,

Alecos Marcides

Mwanasheria - Mshauri